

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

IDARA KUU YA UTUMISHI,

S. L. P. 2483,

Dar es Salaam,

LAAM.

osti, 2002

Kumb. Na EA. 45/257/01

14 April, 2003

WARAKA WA UTUMISHI NA. I WA MWAKA 2003

UTARATIBU WA WATUMISHI WA UMMA WANAOJIUNGA NA  
MAFUNZO KATIKA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

Tangu kuanzishwa kwa Chuo Kikuu Huria Nchini, watumishi wengi wa Serikali wameonesha nia ya kuijunga na mafunzo yatolewayo na chuo hicho. Hadi sasa hakuna mwongozo uliokwishatolewa kuhusu watumishi wanaojiunga na chuo hicho. Kutokana na kukosekana kwa mwongozo, watumishi wengi wamekuwa wakitumia muda wa kazi kwa kujisonea ana maofisini au kwenye Maktaba mbali mbali bila kujali masharti ya ajira zao.

MWONGOZO:

Ili kuweka bayana mazingira mazuri katika watumishi wanaojiunga na mafunzo katika Chuo Kikuu Huria na waajiri inzelekezwa kuwa:

- (i) Mtumishi anapoomba kuijunga na Chuo Kikuu Huria ni lazima apitisha maombi kwa mwajiri wake ili mwajiri ajue kusudio la kuijendeleza kwa mtumishi wake. Hii itamwezesha mwajiri kuweka mazingira mazuri ya kutoa msaada utakaohitajika kwa mtumishi.
- (ii) Mtumishi aliyejiunga na mafunzo hayo bila taarifa atakuwa anakiuka masharti ya kazi yake.
- (iii) Mtumishi anayehudhuria mafunzo ya Chuo Kikuu Huria atastahili likizo maalum wakati wa mitihani ili kumwezesha kufanya mitihani yake. Likizo hiyo haitakatwa katika likizo yake ya mwaka.
- (iv) Hii kuwapa motisha watumishi wanaohudhuria mafunzo, watalipwa shilingi laki mbili (TShs. 200,000/=) kwa ajili ya unumuzi wa vitabu kwa mwaka, Aidha katika mwaka wa mwisho wa mafunzo ambapo intumishi atafanya utafiti wa kumalizia masomo atapewa shilingi laki tatu (TShs. 300,000/=) kumsaidia gharama za utafiti.

BAADA YA KUHITIMU:

Baada ya kumaliza mafunzo watumishi hao wanaweza kuomba kuajiriwa katika fani walizopata sifa kwa kufutata utaratibu ulioelezwa katika Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma. Iwapo walichukua mafunzo ambayo ni ya kada zao wanazofanya kazi wataendelea kufanya kazi zao katika vyeo vyao vya zamani, kwa kuzingatia Miundo ya maendeleo ya Utumishi ambayo imeweka utaratibu wa namna ya kushughulikia watumishi waliojiendeleza kimafunzo.

WAAJIRI:

Waajiri wote wanashauriwa kuwashimiza watumishi wenyewe viwango vya chini vya elimu kuijendeleza kwa kuijunga na Chuo Kikuu Huria ili hatimaye wawze kuboresha utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa Umma. Chuo hicho kina masharti naifuu ya kuijunga na gharama za mafunzo ni naifuu.

Waraka huu uitaanza kutumika tarehe 1 / 7 / 2003.

J. M. RUGUMYAMHETO,  
*Katiba Mkuu (Utumishi)*